INTEGRATED POST PRIMARY EDUCATION PROGRAMME

# ELIMU YA URAIA

## MODULI 2

### Kufafanua Wajibu wa Raia na Serikali



Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

Elimu Changamani Baada ya Msingi

# Kufafanua Wajibu wa Raia na Serikali

unicef
unite for children

Elimu Changamani
baada ya Elimu ya Msingi

INSTITUTE OF ADULT EDUCATION
EDUCATION HAS NO END

**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**
**Elimu Changamani Baada ya Msingi**

S. L. P. 20679,
Dar es Salaam
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed
Tanzania

Pepesi: +255 22 2150836
Barua-pepe: info@iae.ac.tz
Tovuti: www.iae.ac.tz

© Chapa ya Kwanza 2011

**ISBN 978-9987-11-080-3**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya kazi hii kwa namna yoyote isipokuwa kwa kunukuu matini fupifupi zinazoweza kutumika kwa ajili ya utafiti na mapitio ya maandiko, bila kibali cha maandishi kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

# Shukrani

Moduli hii ya **Kufafanua Wajibu wa Raia na Serikali** ni matokeo ya jitihada kubwa za wataalamu mbalimbali kutoka ndani na nje ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW). Mkurugenzi wa TEWW anawashukuru kwa mchango wao muhimu wa muda na rasilimali katika kufanikisha maandalizi ya moduli hii.

Shukurani za pekee zinatolewa kwanza, kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa msaada mkubwa wa fedha na utaalamu. Pili, kwa kikosi kazi cha Mpango wa Elimu Changamani Baada ya Elimu ya Msingi kikiongozwa na Leonia Kassamia (Mratibu) pamoja na Dkt. Wilberforce Meena (Mshauri). Tatu, kwa Dkt. Fidelice Mafumiko Naibu Mkurugenzi (Taaluma, Utafiti na Ushauri) kwa usimamizi imara uliosababisha kufanyika kwa kazi hii kwa ufanisi.

Nne, kwa Bw. E. Samba kwa kuongoza zoezi la uhariri wa kazi hii na Bi. Aneth Katefu kwa kuchapa muswada wa kazi hii. Pamoja na hao, shukurani za dhati zinatolewa kwa waaandishi wafuatao wa moduli hii kwa mchango wao mkubwa walioutoa:

| | |
|---|---|
| Consolata Mongela | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Sedet Bulaya | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |

# Yaliyomo

**Kuhusu Moduli** 1

Muundo wa Moduli ........ 1

**Maelezo ya jumla kuhusu moduli** 3

Karibu katika Moduli ya Elimu ya Uraia: Kufafanua Wajibu wa Raia ........ 3
Umahiri wa Jumla ........ 4
Mbinu za usomaji ........ 4
Unahitaji msaada? ........ 5
Mazoezi ........ 6

**Namna ya kuitumia moduli hii** 6

Ishara za pambizo ........ 6

**Somo la Kwanza** 7

Kueleza Wajibu wa Raia katika Matumizi Salama ya Barabara ........ 7
Utangulizi ........ 7
Matokeo ya kujifunza ........ 7
Dhana ya Usalama Barabarani ........ 7
Vyanzo vya Ajali za Barabarani ........ 10
Matumizi Sahihi ya Barabara ........ 14
Kuzingatia Maelekezo ya Alama za Barabarani ........ 15
Hatua za Kisheria Inapotokea Ajali ........ 17
Tafakuri ........ 20
Zoezi ........ 20

**Somo la Pili** 21

Kutoa Huduma ya Kwanza Inapotokea Ajali ........ 21
Utangulizi ........ 21
Matokeo ya Kujifunza ........ 22
Huduma ya Kwanza ........ 22
Aina Mbalimbali za Ajali ........ 23
Hatua za Huduma ya Kwanza ........ 23
Vifaa vya Huduma ya Kwanza ........ 25
Jinsi ya Kutumia Vifaa vya Huduma ya Kwanza ........ 26

Tafakuri ... 31
Zoezi ... 31

**Somo la Tatu** 32

Kufafanua Madhara ya Dawa za Kulevya na Namna ya Kuepukana Nazo ... 32
Utangulizi ... 32
Matokeo ya Kujifunza ... 32
Dhana ya Dawa za Kulevya ... 33
Madhara ya Dawa za Kulevya ... 33
Kubainisha Njia za Kuepuka Utumiaji wa Dawa za Kulevya ... 34
Tafakuri ... 36
Zoezi ... 36

**Somo la Nne** 37

Kubainisha Misingi ya Utawala Bora na Maadili ... 37
Utangulizi ... 37
Matokeo ya kujifunza ... 37
*Kueleza Dhana ya Utawala Bora* ... 38
Kubanisha Misingi ya Utawala Bora ... 38
Kueleza Dhana ya Maadili ya Uongozi ... 39
Kuanisha Misingi ya Maadili ya Uongozi Bora ... 40
Kutathmini Hali ya Utawala Bora na Maadili ya Uongozi katika Jamii ... 41
Tafakuri ... 43
Zoezi ... 43

**Somo la Tano** 45

Kubainisha Misingi ya Utandawazi na Namna ya Kukabiliana na Changamoto Zake .. 45
Utangulizi ... 45
Matokeo ya kujifunza ... 45
Dhana ya Utandawazi ... 45
*Chimbuko* la Utandawazi ... 46
Misingi ya Utandawazi ... 47
Manufaa na Changamoto za Utandawazi ... 48
Tafakuri ... 50
Zoezi ... 50
Marejeo ... 52

# Kuhusu Moduli

Moduli ya Elimu ya Uraia : Kufafanua Wajibu wa Raia imetayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Moduli zote zilizotayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima zina muundo sawa, kama ilivyoelezwa hapa chini.

## Muundo wa Moduli

### Maelezo ya jumla kuhusu moduli

Maelezo ya jumla kuhusu moduli hutoa utangulizi wa jumla wa Moduli. Habari zinazopatikana katika maelezo ya jumla kuhusu Moduli zitakusaidia kuamua:

- kama moduli hii inakufaa kama moduli hii inakufaa;
- kile unachohitajika kukijua kabla ya moduli hii;
- unachoweza kutarajia kutoka kwa Moduli;
- muda utakaohitaji ili kukamilisha Moduli;

Maelezo haya ya jumla pia hutoa mwongozo juu ya:

- mbinu za usomaji;
- mahali pa kupata msaada;
- mazoezi ya nyumbani na tathmini;
- ishara za vitendo mbalimbali; na
- masomo.

Tunatilia mkazo ushauri kwamba usome maelezo ya jumla kuhusu Moduli *kwa makini* kabla ya kuanza masomo yako.

### Yaliyomo kwenye Moduli

Moduli hii imegawanywa katika masomo. Kila somo lina:

- utangulizi wa yaliyomo kwenye Moduli;
- matokeo ya somo;
- istilahi mpya;

maudhui ya kimsingi ya somo pamoja na mazoezi mbalimbali ya kusoma;

muhtasari wa somo; na

mazoezi ya nyumbani na/au tathmini, kama inavyohitajika.

## Marejeo

Kwa wale wanaopenda kujifunza mengi juu ya mada hii, tunawapa orodha ya marejeo ya ziada mwishoni mwa moduli hii; haya yanaweza kuwa vitabu, makala au tovuti.

## Maoni yako

Baada ya kukamilisha moduli ya Elimu ya Uraia : Kufafanua Wajibu wa Raia tutashukuru ikiwa utatenga muda mfupi kutupa maoni yako kuhusu kipengele cho chote cha moduli hii. Maoni yako yanaweza kuhusu:

- yaliyomo kwenye moduli na muundo wake;
- makala za kusoma za moduli na marejeo mengine;
- mazoezi ya nyumbani ya moduli;
- tathmini za modul;
- muda wa moduli;
- msaada katika moduli (wahadhiri waliosimamia moduli, msaada wa kiufundi, n.k.)
- ukitoa maoni mwafaka utatusaidia kuboresha moduli hii.

# Maelezo ya jumla kuhusu moduli

## Karibu katika Moduli ya Elimu ya Uraia: Kufafanua Wajibu wa Raia na Serikali

Ndugu mwanafunzi, karibu katika masomo ya moduli hii ya 'Wajibu wa Raia' ambayo ni ya pili katika Elimu ya Uraia. Moduli hii ina jumla ya masomo matano kama ifuatuatavyo: Matumizi Salama ya barabara; Huduma ya kwanza; Madhara ya Dawa za Kulevya; Misingi ya Utawala Bora, Maadili ya Uongozi; na Misingi ya utandawazi.

Ninakushauri ujiwekee malengo na ratiba ya kujifunza moduli zako zote ulizoamua kuzisoma. Unatarajiwa kumaliza moduli hii ya Elimu ya Uraia katika muda usiozidi saa 30. Hii ina maana kuwa katika mpango wa ratiba yako ya kujifunza, weka nafasi ya idadi hiyo ya saa. Kulingana na hali yako halisi, inawezekana kabisa ukamaliza moduli hii chini ya muda huo au zaidi kidogo.

Ili kurahisisha kazi ya kuweka kumbukumbu ya maendeleo yako ya kujifunza, ninakushauri pia uwe na kifaa kinachoitwa 'mkoba wa kazi'. Mkoba wa kazi ni bahasha kubwa, kabrasha au jalada ambamo mwanafunzi anaweka nakala za mazoezi anayoyafanya mwanzoni, katikati au mwisho wa somo, muhtasari wa maarifa zaidi unayojitafutia juu ya somo kutokana na kusoma matini, vitabu, magazeti, vijarida, vipeperushi, chati, kuangalia televisheni, kusoma kupitia intaneti.

Mwishoni mwa kila somo utakutana na vikipengele vya *tafakuri* na *tathmini* ambavyo utavitumia kujipima ni kiasi gani umeweza kupata umahiri uliokusudiwa kwa mfano matokeo ya mafunzo katika somo husika. Pia maendeleo yako yatapimwa kupitia, mazoezi/au kazi na majaribio ambayo yatatolewa na mwezeshaji wako, ambaye atayasahihisha na kukurudishia.

## Umahiri wa Jumla

Kushiriki kikamilifu katika masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kuzingatia haki za binadamu.

## Mbinu za usomaji

Kwa kuwa wewe ni mwanafunzi wa Elimu Changamani Baada ya Msingi, utaratibu wako wa kusoma utakuwa tofauti na ule ulioutumia ulipokuwa bado shuleni: utachagua unachotaka kusoma, utakuwa na motisha ya kitaalamu na/au ya kibinafsi inayokusukuma, na bila shaka utakuwa ukiratibu shughuli zako za kiusomaji huku ukizingatia majukumu yako mengine ya kitaalamu au kinyumbani.

Kimsingi, utakuwa unayadhibiti mazingira yako ya masomo. Kwa hivyo, utahitajika kufikiria juu ya maswala ya utendaji yanayohusiana na udhibiti wa wakati, kuweka malengo, udhibiti wa shinikizo, n.k. Pengine utahitaji kujizoesha tena katika maeneo kama upangaji wa insha, namna ya kuimudu mitihani, na kutumia mtandao kama marejeo ya ujifunzaji.

Mambo utakayozingatia sana ni *muda* na *nafasi*, yaani muda unaotenga kwa masomo yako na mazingira unamosomea.

Tunapendekeza kwamba uchukue nafasi hii – kabla ya kuanza kujisomea kibinafsi – kujifahamisha mambo haya. Kuna marejeo mengi mazuri kwenye mtandao. Viungo vichache vinavyopendekezwa ni:

http://www.how-to-study.com/

Tovuti ya "How to study" yaani "Jinsi ya kusoma" imetengwa mahsusi kwa ajili ya marejeo ya mbinu za usomaji. Utapata viungo kuhusu kujitayarisha kusoma (orodha ya mambo tisa muhimu kuhusu mahali pazuri pa kusomea), kuandika kumbukumbu, mikakati ya kusoma vitabu vya kiada, kutumia vyanzo vya kumbukumbu, dukuduku la mitihani.

http://www.ucc.vt.edu/stdysk/stdyhlp.html

Hii ni tovuti ya Kitengo cha Masuala ya Wanafunzi, Virginia Tech. Utapata viungo vya namna ya kupanga muda wako (ikiwa ni pamoja na kiungo cha "wakati huenda wapi?"), orodha-kaguzi ya

mbinu za usomaji, mbinu za kimsingi za kumakinikia jambo, udhibiti wa mazingira ya kusomea, kuandika kumbukumbu, namna ya kusoma insha kwa kusudi la kuchanganua, mbinu za kukumbuka.

http://www.howtostudy.org/resources.php

Hii ni tovuti nyingine ya "jinsi ya kusoma" iliyo na viungo muhimu kuhusu udhibiti wa wakati, kusoma kwa ufanisi, mbinu za kusaili/kusikiliza/kuchunguza, kufaidi kutokana na kutenda (ujifunzaji wa kiutendaji), kukuza kukumbuka, vidokezo vya namna ya kudumisha motisha, kukuza mpango wa ujifunzaji.

Viungo vilivyo hapo juu ni mapendekezo yetu ya kukuwezesha kuanza. Wakati tulipokua tukiandika, viungo vya tovuti hizi vilikuwa vinatumika. Ikiwa unataka kupata tovuti zaidi, nenda kwa www.google.com kisha upige taipu na kutafuata "self-study basics" (misingi ya usomi wa kibinafsi), "self-study tips" (vidokezo vya usomi wa kibinafsi), "self-study skills" (mbinu za usomi wa kibinafsi) au tovuti nyingine zenye mada kama hizo.

## Unahitaji msaada?

Mpendwa mwanafunzi, katika mchakato wako wa kujifunza, unaweza kuhitaji msaada kuhusu mambo mbalimbali, kwa mfano, mahali unapoweza kupata msaada na namna ya kupata msaada huo. Pamoja na hayo, unaweza kuhitaji ufafanuzi kuhusu moduli unazosoma. Hivyo basi, unashauriwa kuomba ufafanuzi wa yote hayo kwa mratibu wa kituo chako au mwezeshaji wako. Pia, unaweza kufungua tovuti ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima yenye anwani hii: www.iae.ac.tz au piga simu hii +255 22 2150836.

## Mazoezi

Baada ya kila somo, unahitajika kujibu maswali ya zoezi la somo. Majibu ya zoezi hili la kila somo hautayawasilisha kwa mwezeshaji wako, ni kwa ajili ya kufanya tafakuri ya ulichojifunza. Pia, utapewa majaribio na mazoezi ambayo utayafanya na kuyawasilisha kama utakavyoongozwa na mwezeshaji wako. Pamoja na hayo, utatakiwa kufanya mitihani ya majaribio kwa ajili ya upimaji wa maendeleo yako ya kitaaluma.

# Namna ya kuitumia moduli hii

## Ishara za pambizo

Huku ukifanya kazi katika moduli hii utagundua kwamba kuna matumizi mengi ya ishara za pambizo. Ishara hizi zina jukumu la kushiria aina fulani ya matini, kazi mpya au kubadilika kwa zoezi. Zimetumiwa ili kukuongoza ujue namna ya kuitumia moduli hii.

Seti nzima ya ishara imetolewa hapa chini. Tunapendekeza kuwa ujizoeze ishara hizi na maana yake kabla ya kuanza masomo yako.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Zoezi | Tathmini | Zoezi la Somo | Kisa Mafunzo |
| Mjadala | Zoezi la Kikundi | Usaidizi | Kumbuka! |
| Matokeo | Kusoma | Tafakuri | Mbinu za Usomaji |
| | Istilahi | Muda | Kidokezi |

# Somo la Kwanza

## Kueleza Wajibu wa Raia katika Matumizi Salama ya Barabara

### Utangulizi

Nchini Tanzania kumekuwa na matukio mengi mbali mbali ya ajali za barabarani, ambayo yamekuwa yakiripotiwa na vyombo vya habari. Ni wazi kwamba kuna mambo mengi yanayosababisha ajali hizi. Kubwa miongoni mwake ni watu kutotumia barabara kwa usahihi. Hivyo basi, katika somo hili tutajifunza juu ya wajibu wa raia katika matumizi salama ya barabara kwa ajili yako na raia wengine.

## Matokeo ya kujifunza

Ndugu mwanafunzi, utakapokuwa unakamilisha kujifunza somo hili, unakusudiwa uwe umepata umahiri wa:

- kueleza kwa usahihi dhana ya usalama barabarani;
- kubainisha vyanzo na sababu za ajali barabarani ;
- kutumia barabara kwa usahihi ;
- kuzingatia maelekezo ya alama za barabarani mahali pale zinapokuwepo; na
- kuchukua hatua za kisheria ajali inapotokea.

### Dhana ya Usalama Barabarani

Je, umewahi kuhusika katika ajali ya aina yoyote barabarani, au, kuishuhudia? *Kama ulihusika au kushuhudia:* Ajali hiyo ilisababishwa na nini na makosa yalikuwa ya nani? Kwa kiasi gani alama za barabarani, kama zilikuwepo, zilizingatiwa au hazikuzingatiwa? Hatua zipi, zilichukuliwa? Kama hakuna hatua zozote zilizochukuliwa, unadhani ni kwanini?

Siku moja, baada ya tangazo moja la ajali kutangazwa redioni ambapo watu walipoteza uhai na wengine wengi kujeruhiwa, palitokea mjadala kati ya wanafunzi wawili. Majadiliano yalikwenda kama ifuatavyo:

**Zawadi:** Baraka, mbona ajali za barabarani nchini mwetu zimezidi, sababu ni nini?

**Baraka:** Ni kweli kabisa Zawadi. Kumekuwa na matukio mengi sana ya ajali barabarani. Lakini naona kabla hatujafikilia vyanzo, hebu kwanza tuangalie dhana ya usalama barabarani.

**Zawadi:** Ninavyoelewa mimi, usalama barabarani maana yake ni ile hali ya mtu kutumia barabara kusafiri toka sehemu moja hadi nyingine bila kudhurika kwa namna yoyote kutokana na vyombo vinavyotumia barabara. Barabara inaweza kuwa kuu au ndogo inayotoka au kuingia katika barabara kuu.

Ndugu mwanafunzi, nina hakika mazungumzo haya yamekupa dhana ya usalama barabarani kwa kiasi fulani. Kabla hatujaendelea mbele, hebu angalia picha hapo chini.



Gari ndogo





Pick up




Gari la kubebea wagonjwa



Basi





Trekta

Bajaji



Pikipiki



Baiskeli ya magurudumu mawili



Baiskeli ya magarudumu matatu

---

Je, unavifahamu vyombo vyote? Andika majina yake kwa kufuata mpangilio wa namba. Vyombo vipi kati ya hivyo vinahusika sana katika matukio ya ajali ulizozishuhudia au kuzisikia? Unadhani ni kwa nini?

---

Bila shaka umeweza kuyajibu maswali yote juu ya Picha Namba 1.

Endapo umeona ugumu au umekuwa na mashaka juu ya baadhi ya majibu, nakushauri uyatafute kwa marafiki, ndugu au wanajamii wengine wanaoyafahamu. Ukishayakamilisha yaweke ndani ya mkoba wa kazi.

Hapa umefika mwisho wa sehemu ya pili ya somo la kwanza la Moduli ya Wajibu wa Raia. Jitayarishe kuingia katika sehemu inayofuata.

*Unavijua vyanzo vya ajali za barabarani?*

## Vyanzo vya Ajali za Barabarani

Wakati Zawadi na Baraka wakiendelea na majadiliano yao, alitokea afisa usalama barabarani aliyekuwa ameyasikiliza maongezi yao toka mwanzo. Alivutiwa na kuwasogelea baada ya kuwasikia wakibishana juu ya vyanzo vya ajali barabarani. Mmoja wao alikuwa anasisitiza kuwa ajali barabarani zinasababishwa na uzembe wa madereva peke yao. Hivyo, afisa usalama huyo aliamua kuwasuluhisha kwa kuwaeleza kuwa vyanzo vya ajali barabarani ni pamoja na:

1. madereva wa vyombo vya moto;
2. vyombo vyenyewe;
3. waendeshaji wa vyombo visivyo vya moto;
4. watembea kwa miguu;
5. wanyama; na
6. barabara zenyewe.

Afisa huyo aliendelea kuelezea sababu za ajali barabarani kwa kuzianisha kufuatana na kila chanzo.

**Madereva wa vyombo vya moto**

Alisema kuwa chanzo hiki, mara nyingi, husababisha ajali barabarani kutokana na yafuatayo:

1. kuendesha bila kuwa na umahiri wa kuendesha chombo husika;
2. kuendesha chombo bila kuzingatia sheria na alama za barabarani;
3. kuendesha chombo kibovu, kwa mfano chombo hakina breki, taa za ishara ya muelekeo, taa za kuonea usiku, vioo vya pembeni mwa gari na honi;
4. kuendesha chombo akiwa amelewa;
5. kuendesha chombo huku akitumia simu ya mkononi;
6. Kuendesha chombo akiwa amechoka sana, anamsongo wa mawazo, anuamwa au ana matatizo ya macho.
7. Kuegesha, gari bovu pembeni mwa barabara bila kuweka vifaa (viakisi) vinavyoonesha kuwepo gari bovu mahali hapo.

Afisa usalama aliendelea kuwaeleza kuwa, wajibu wa raia ni kuzingatia yafuatayo unapoendesha vyombo vya moto:

- uwe mahiri katika kuendesha. Kwa mfano, uwe na leseni inayotambuliwa na kuthibitishwa na vyombo halali vya serikali,
- kujua na kuzingatia sheria na alama za barabarani;
- usiendeshe chombo kibovu;
- unapoendesha usilewe, au usiendeshe ukiwa umelewa;
- usitumie simu ya mkononi wakati unaendesha;
- Epuka kuendesha wakati umechoka sana, una usingizi, una msongo wa mawazo, unaumwa au uono na usikivu hafifu; na
- Tumia viakisi ili kuonesha kuwa chombo kibovu kimeegeshwa pembeni badala ya matawi ya miti yasiyoonekana.

Vyombo vyenyewe

Afisa Usalama alisema kwamba, ukiwa raia, wajibu wako ni kufanya yafuatayo:

- chombo kikaguliwe kabla ya kuanza safari;
- zingatia kupeleka chombo kwa ajili ya ukaguzi kama inavyotakiwa;
- kuwepo mikanda kwa ajili ya kufunga wanaosafiri; na
- hakikisha chombo chako kina vipuri vya kutosha uwapo safarini.

Hapa, afisa alieleza kuwa sababu za ajali zinazotokana na chanzo hiki ni chombo kupata ubovu ghafla wakati kipo katika mwendo. Kwa mfano: kukatika breki; kupasuka gurudumu au magurudumu; kukatika usukani; na kuzimika taa ghafla hasa wakati wa usiku.

***Waendeshaji wa vyombo visivyo vya moto***

Chanzo hiki, alisema, kinasababisha ajali barabarani kutokana na mtu:

1. kuendesha chombo bila taa usiku;
2. kukatizakatiza barabara ni ovyo mahali pasipofaa;
3. kuendesha chombo kisicho na breki na/au kengele;
4. kuendesha chombo kwa kuyumbayumba barabarani, aidha, kwa madoido tu, ulevi au kutojua kuendesha;
5. kupakia abiria wanaozidi uwezo wa chombo;
6. kuvuka barabara bila kuangalia, kulia na kushoto, kulia tena;
7. kuvuka wakati taa za kijani zinawaka;
8. kuvuka kwa mshazali;

9. kuendesha upande wa barabara usio sahihi; na
10. kubeba mizigo mirefu au mipana bila alama ya tahadhari.

Baada ya kueleza kuhusu waendesha vyombo visivyo vya moto, Afisa Usalama aliwaeleza kuwa, ili kuepuka ajali zinazosababishwa na vyombo visivyo vya moto raia unapaswa kuzingatia yafuatayo :

- hakikisha chombo chako kina vifaa vyote vinavyotakiwa kama vile taa, breki n.k ;
- usikatizekatize barabara bila mpango;
- usinywe na kuendesha na usiendeshe ukinywa;
- pakia mzigo unaotakiwa, usizidishe ;
- vuka barabara kwa uangalifu kwa kufuata sheria ;
- zingatia taratibu za kuvuka barabara mahali palipo na taa;
- usivuke barabara kimshazali ;
- Fuata upande wako wa kuendeshea.

***Watembea kwa miguu***

Watembea kwa miguu nao ni chanzo kinachosababisha ajali barabarani kwa njia zifuatazo:

1. kuvuka barabara bila kuangalia kulia, kushoto na kulia tena;
2. kuvuka wakati taa za kijani zinawaka;
3. kuvuka kwa mshazali;
4. kuvuka kwa kukimbia ;
5. kuvuka mbele ya gari lililoegeshwa;
6. kutembea upande wa barabara usio sahihi na kwa kujitandaza;
7. kuyumbayumba barabarani, aidha, kwa ulevi au ugonjwa;
8. kubeba mizigo iliyotanda pande mbili na kuchukua sehemu kubwa ya barabara bila alama ya tahadhali; na
9. kuvuka ukidhani barabara ni moja mahali ambapo kuna barabara mbili au tatu." Hapa, afisa usalama barabarani alinyamaza kidogo, akawakazia macho kisha akawauliza, *"Ninyi mkiwa katika barabara za aina hii mtafanyaje?"*

Afisa Usalama, aliwaasa watembea kwa miguu kuzingatia mambo yafuatayo:

- angalia kulia, kushoto na kulia tena;

- zingatia taratibu za kuvuka barabara mahali palipo na taa za barabarani;
- epuka kuvuka kwa mshazari, vuka kwa wima ;
- hakikisha hakuna kitu kinachokukinga kulia na kushoto unapovuka;
- tembea upande wa barabara unaotakiwa (kushoto);
- epuka ulevi unapotembea barabarani;
- epuka mizigo inayotanda barabarani kwa upana na urefu; na
- tafuta msaada iwapo hufahamu matumizi ya barabara zinapokuwa zaidi ya moja.

Kwa kutumia maarifa waliyokwishapata katika maelezo yake, walimjibu naye akaridhika, akaendelea na vyanzo vilivyobaki.

***Wanyama***

Baadhi ya ajali husababishwa na wanyama wanapokatiza barabara ghafla au kuvushwa na wachungaji kwenye kona kali.

Afisa Usalama alielezea zaidi kuwa ukiwa raia unapaswa kufanya yafuatayo kuhusiana na wanyama:

- usipitishe wanyama kwenye barabara ; na
- kuwa mwangalifu kwenye alama zinazoonesha mapito ya wanyama kama vile Ranchi za Mifugo, Mbuga za Wanyama.

***Barabara***

Barabara inaweza kuwa chanzo cha ajali barabarani pale inapokuwa:

- haina alama za kuelekeza watumiaji;
- na mashimo makubwa, hasa yaliyojaa maji; na
- miti na nguzo pembezoni ambazo zinaweza kuanguka ghafla kwa upepo, mvua, tetemeko au kuoza;
- utelezi

Afisa alimalizia kwa kusema kuwa, wajibu wa raia wako kuhusu wanyama ni:

- endesha polepole na kwa ungalifu kama barabara ni mbovu au kuna miti au nguzo pembezoni mwa barabara;

- kuwa mwangalifu sehemu za madaraja hasa wakati wa mvua kwani mengine huweza kubomoka/kuvunjika iwapo lilikuwa na ubovu; na
- kuwa makini kwenye barabara ambazo nyaya za umeme zimekatiza.

Afisa alipomaliza kueleza, Zawadi na Baraka walimshukuru sana kwa maelezo yake mazuri.

---

Baada ya kusoma maelezo ya mtaalamu juu ya vyanzo na sababu ya ajali barabarani, jadili na marafiki au ndugu jinsi ambavyo ungejibu swali alilowauliza Zawadi na Baraka; vyanzo na sababu nyingine zaidi za ajali barabarani.

---

Majibu utakayoyapata yaandike na uyahifadhi katika mkoba wa kazi.

Baada ya kufanya kazi hii, utakuwa umekamilisha sehemu ya pili ya somo la kwanza la Moduli ya Wajibu wa Raia. Kwaheri, na jitayarishe kuingia katika sehemu inayofuatia.

## Matumizi Sahihi ya Barabara

Ndugu mwanafunzi, baada ya kuwa umebainisha vyanzo na sababu za ajali barabarani, je sasa unaweza kutumia barabara kwa usahihi? Toa sababu za jibu lako. Jadiliana na rafiki au jamaa zako kisha uandike kwa kifupi matumizi sahihi ya barabara.

Bila shaka hamtakuwa mbali na baadhi ya haya yafuatayo:

- kuzingatia alama za barabarani;
- kuwaheshimu na kuwajali watumiaji wengine wa barabara;
- Matumizi sahihi ya taa za kuongoza magari kwa watumiaji wa mjini: taa nyekundu inaamrisha magari **kusimama**; taa ya kijani inaruhusu magari **kwenda**; na taa ya njano inataarifu magari **yajitayarishe kusimama au kwenda;**
- kukaa pembeni inapotokea dharura. Kwa mfano, magari ya wagonjwa, msafara wa viongozi wa kitaifa na magari ya zima moto; hata kama sheria au alama inakuruhusu;
- unapovuka reli inayokatisha barabara, kuwa mwangalifu kwani treni daima haigongi bali inagongwa;
- kupita upande wa kulia wa barabara unapotembea kwa miguu au kwa chombo kisicho cha moto; pia kupita kushoto kama unaendesha chombo cha moto. Hii ni kulingana na sheria za

barabara kwa Tanzania. Katika baadhi ya nchi, vyombo vya moto hupita mkono wa kulia, ambapo watembea kwa miguu na vyombo visivyo ya moto hupita kushoto; na

- kuwasaidia wasiojiweza wavuke salama, kwa mfano wazee, watoto na wasioona, kwa kuwashika mkono.

---

Toa maoni yako juu ya faida, au hasara, ya kanuni ya watembea kwa miguu au watumiaji wa vyombo visivyo vya moto kupita upande wa kulia nchini mwetu. Weka maoni yako katika mkoba wa kazi.

---

Baada ya kufanya kazi hii, ndugu mwanafunzi, utakuwa umekamilisha sehemu ya tatu ya somo la kwanza la Moduli ya Wajibu wa Raia. Kwaheri, na jitayarishe kuingia katika sehemu inayofuatia.

## Kuzingatia Maelekezo ya Alama za Barabarani

Ndugu mwanafunzi, hebu rejea sehemu ya tatu ya somo la 'Kutumia barabara kwa usahihi'. Utaona kuwa njia mojawapo ya kukuwezesha kutumia barabara kwa usahihi ili kujikinga na ajali, ni kuzingatia alama za barabarani.

Sasa tazama picha inayoonesha baadhi ya alama za usalama barabarani na fasiri zake.

**Picha Na. 2**



**Baadhi ya Alama za barabarani**

**fasiri ya alama za barabarani katika picha**

| | |
|---|---|
| 1. Mkokoteni hauruhusiwi | 1. Usipige honi |
| 2. Simama: Makutano ya barabara kuu | 2. Mbele kuna mto |
| 3. Marufuku kupita hapa | 3. Mbele kuna mteremko mkali |
| 4. Marufuku waenda kwa miguu kupita hapa | 4. Mbele kuna mwinuko mkali |
| 5. Marufuku Magari marefu zaidi ya mita 10 kupita hapa | 5. Mbele kuna kona kali kulia |
| 6. Tumia barabara yoyote | 6. Mbele kuna hatari nyingine |
| 7. Mbele kuna kivuko cha waendesha baskeli | 7. Mbele barabara ina matuta |
| 8. Marufuku baskeli kupita hapa | 8. Makutano ya T mbele |
| 9. Marufuku kulipita gari la mbele yako | 9. Mbele reli inakatisha kuna lango |
| 10. Marufuku kugeuza na kurudi unakotoka | 10. Mbele kuna barabara kulia inayoingia barabara kuu |
| 11. Mbele kuna barabara kushoto inayoingia barabara kuu | 11. Mbele kuna makutano ya barabara |
| 12. Marufuku Kupinda kushoto | 12. Mbele kuna mzunguko au kisiwa |
| 13. Fuata mshale | 13. Pinda kulia |
| 14. Usiegeshe gari | 14. Mbele kuna barabara yenye njia mbili |
| 15. Marufuku Kupinda kulia | 15. Mbele kuna kivuko cha mifugo |
| 16. Usivute sigara | 16. Mbele kuna hifadhi ya wanyama pori |
| 17. Chepuka kushoto | 17. Mbele kuna Taa za kuongoza magari |
| 18. Marufuku baiskeli na magari kupita hapa | 18. Marufuku waendao kwa miguu kipita hapa |
| 19. Simama | 19. Mbele barabara inateleza |
| 20. Mbele barabara ndogo inakatisha barabara kuu | 20. Mbele reli inakatisha barabara |
| 21. Pisha njia | 21. Mbele kuna kiwanja cha ndege |

Ndugu mwanafunzi, baada ya kuwa umekwishatazama alama hizi na kusoma tafsiri zake vizuri, zichanganue katika makundi sita yafuatayo:

- alama zinazowalenga zaidi waenda kwa miguu na vyombo visivyo vya moto;
- alama zinazowalenga zaidi waendesha vyombo vya moto;
- alama zinazolenga makundi yote mawili A na B;
- alama zinazotoa amri;
- alama zinazotoa tahadhari;
- alama zinazotoa taarifa; na
- alama zilizo katika sehemu unayoishi na/au kutembelea mara kwa mara.

Jadili na wanafunzi wenzako walio karibu nawe au ndugu na marafiki zako. Majibu utakayoyapata weka kwenye mkoba wa kazi. Kama ukibahatika kukutana na afisa yeyote wa usalama barabarani muoneshe akusaidie kuona kama uko sahihi au la. Mwombe akuelekeze jinsi ya kupata chati ya alama zote za usalama barabarani, inayotolewa kwa hisani ya 'Huduma ya Wasafiri Tanzania', toleo linalotumika. Katika kipindi cha ana kwa ana, muoneshe mwezeshaji atakusaidia pia.

Baada ya kufanya kazi hii, utakuwa umekamilisha sehemu ya nne ya somo la kwanza la Moduli ya Wajibu wa Raia. Jitayarishe kuingia katika sehemu inayofuatia.

## Hatua za Kisheria Inapotokea Ajali

Ndugu mwanafunzi, karibu katika sehemu hii ya tano na ya mwisho ya somo la kwanza la Moduli ya Wajibu wa Raia.

Katika sehemu ya kwanza ya somo hili nilikuuliza iwapo ulikwisha husika au kushuhudia ajali barabarani, na hatua zipi ulichukua au zilichukuliwa. Nilikuuliza pia kuwa kama hapakuwa na hatua yoyote iliyochukuliwa, ilikuwa ni kwa nini.

Hebu soma kisa mafunzo kifuatacho kwa makini uone ni kwa kiasi gani majibu uliyoyatoa yanapatikana humo.

Siku moja, nilikuwa nasafiri kutoka Kijiji cha Ngerengere, kuelekea nyumbani Mikese. Nilipanda basi liitwalo Mtukwao Trans. Dereva wetu alikuwa akiendesha gari kwa mwendo kasi. Baadhi ya abiria tulijaribu kumwonya na kumsihi apunguze mwendo. Badala ya kutusikiliza, aliongeza mwendo. Haukupita muda tukafika kwenye makutano ya kuingia barabara kuu ya Dar es Salaam - Morogoro. Dereva aliingia barabara kuu bila kusimama na akamgonga mwendesha baskeli aliyekuwa katika hiyo barabara kuu. Mwendesha baskeli alikuwa amebeba abiria mmoja. Katika harakati za kujaribu kumkwepa mwendesha baskeli, basi lilipinduka na abiria kumi walijeruhiwa. Wawili kati yao walijeruhiwa vibaya sana. Mwendesha baskeli aliyegongwa alivunjika mguu, na abiria wake alivunjika mkono.

Kwa vile sehemu hiyo ilikuwa karibu na kijiji, wanakijiji walijikusanya na kutaka kuanza kumpiga dereva wa basi ambaye tulikuwa tumemshikilia ili asikimbie. Tulijitahidi kuwazuia wanakijiji hao wasimpige japo alikuwa na makosa. Mimi nilipiga simu polisi haraka kwa kutumia namba ya dharura ya polisi. Je, unajua namba ya dharura ya polisi. Tafadhari itafute kwani ni muhimu kuwa nayo. Kwa bahati, askari wa usalama barabarani nao walifika mara, wakiambatana na gari la wagonjwa. Walipofika tu, Askari watatu kati yao walianza kusaidiana na wauguzi kuwakagua majeruhi. Baada ya kupatiwa huduma ya kwanza, walioumia sana walichukuliwa katika gari la wagonjwa. Kwa wale wenye nafuu, wakapelekwa hospitali kwa usafiri mwingine wakiwa na askari mmoja.

Askari mwingine, aliyeonekana kuwa kiongozi wao, alimwendea dereva moja kwa moja; akakagua leseni yake; bima ya gari; na leseni ya barabara. Vitu vyote aliviona viko sawasawa. Ndipo akaanza kuwauliza abiria juu ya kilichotokea. Alielezwa kuwa dereva alikuwa anakwenda mwendo kasi na hakusimama alipofika kwenye makutano ya barabara kuingia barabara kuu.

Baada ya kuchukua maelezo yote, dereva alipelekwa kituo cha polisi na kufunguliwa mashtaka. Alikaa rumande hadi majeruhi wote waliporuhusiwa kutoka hospitali. Kwa kuwa alipatikana na makosa, alinyang'anywa leseni na kuamuliwa kifungo cha miezi sita jela. Majeruhi wote katika ajali, na yule mwendesha baiskeli na abiria wake walilipwa fidia kutokana na bima ya basi lililohusika na ajali.

Ndugu mwanafunzi, natumaini umekielewa vema kisa mafunzo hiki.

Baaada ya kisa hiki sasa fanya yafuatayo:

---

Orodhesha hatua zote za kisheria zilizochukuliwa katika tukio zima. Zimo hatua zisizopungua saba.

Ni mambo gani ambayo yangeweza kufanya hatua hizo zote au baadhi yake zisichukuliwe na/au kutekelezwa kikamilifu? Jadili na wana mafunzo wenzako waliokaribu nawe au ndugu na marafiki zako kisha weka majibu katika mkoba wa kazi. Mtajadiliana zaidi na mwezeshaji mkiwa ana kwa ana.

---

Baada ya kufanya hayo yote, utakuwa umefikia tamati ya somo la 'Matumizi ya barabara kwa usalama wako na watu wengine', ila utafanya tafakuri na tathmini yake kabla ya kuanza somo la pili.

## Tafakuri

Mambo gani umejifunza katika somo zima? Ni kipengele kipi katika somo hili kimekuwa kivutio zaidi kwako na kwa nini? Wapi umekutana na ugumu wa kujifunza somo hili? Ni hatua gani umechukua au utachukua ili kuweza kupata ufumbuzi wa tatizo au matatizo yako?

## Zoezi

Ndugu mwanafunzi, bila shaka sasa unaweza kujipima kama matokeo ya mafunzo yaliyokusudiwa yameweza kufikiwa kufuatana na mwongozo wa maswali yafuatayo:

1. Nini maana ya usalama barabarani?
2. Bainisha vyanzo na sababu za ajali barabarani.
3. Taja hatua za kisheria unazoweza kuchukua inapotokea ajali.

# Somo la Pili

## Kutoa Huduma ya Kwanza Inapotokea Ajali

### Utangulizi

Ndugu mwanafunzi, karibu sana katika somo la pili la Moduli ya Elimu ya Uraia. Rejea somo letu la kwanza tuliposoma kisa mafunzo kilichohusu ajali iliyowahi kutokea mahali fulani. Katika ajali hiyo, inaelekea majeruhi hawakuwa wamepatiwa msaada wowote hadi wauguzi walipofika pamoja na askari wa usalama barabarani. Hebu jiulize askari na wauguzi hao wangechelewa kufika mahali pa ajali nini kingeweza kutokea? Unadhani ni kwanini msaada wowote wa huduma ya kwanza haukutolewa na abiria ambao hawakuwa wameumia wala wanakijiji waliokusanyika?

Ni wazi kwamba huduma ya kwanza ni muhimu kwa kila mtu anapoumia katika ajali ya aina yoyote ile na mahali popote, bila kuchelewa. Kama hivyo ndivyo, ina maana kila mwanajamii anatakiwa kuwa na ujuzi wa kutoa huduma hiyo. Ni kwa sababu hii, somo hili linalenga kukunufaisha /kukufahamisha wajibu wako kama raia na kukupatia umahiri wa kutoa huduma ya kwanza ajali inapotokea.

# Matokeo ya Kujifunza

Ndugu mwanafunzi, utakapokuwa una kamilisha kujifunza somo hili, unakusudiwa uwe umepata umahiri katika maeneo yafuatayo:

- kubainisha dhana ya huduma ya kwanza kwa usahihi;
- kuainisha aina mbalimbali za ajali ;
- kueleza hatua za kuchukua kulingana na aina ya ajali ;
- kuanisha vifaa muhimu vya huduma ya kwanza kwa aina mbalimbali za ajali; na
- kutumia vifaa vya huduma ya kwanza kumuhudumia aliyepata ajali.

## Huduma ya Kwanza

Ndugu mwanafunzi, karibu katika sehemi hii ya kwanza katika somo la pili la Moduli ya Wajibu wa Raia.

Katika sehemu hii utajifunza juu ya dhana ya huduma ya kwanza jinsi ya kutoa huduma ya kwanza jinsi ya kutoa huduma hiyo katika mazingira mbalimbali.

Huduma ya kwanza ni msaada wa haraka anaopatiwa mtu aliyeumia au kuugua ghafla kabla ya kupelekwa hospitali au kituo cha afya kupatiwa matibabu kamili. Lengo la msaada huo ni kumpunguzia maumivu na/au kuzuia hali isiwe mbaya zaidi.

Ndugu mwanafunzi, kama ulivyoona katika picha, huduma ya kwanza haihitaji gharama kubwa kuitoa. Wakati mwingine inaweza kuwa ni kumfanyia mwathirika mambo yafuatayo tu:

- kummwagia, kumlowesha au kusafisha kwa maji safi;
- kumfungua vifungo, tai, mkanda kiunoni, na kumvua viatu;
- kumpepea; na
- kumweka kivulini, na kadhalika.

Haya yote hutegemeana na aina ya ajali au ugonjwa.

Sasa jaribu kuyafikiria matukio ambapo huduma kama hiyo ilitolewa, ama, na wewe mwenyewe au watu wengine na baadaye mwathirika kupelekwa hospitali/kituo cha afya, na pengine kupona kabisa. Orodhesha na kuelezea kila tukio kwa kifupi kasha uiweke katika mkoba kazi wako.

Ndugu mwanafunzi, baada ya kufanya hayo, utakuwa umemaliza sehemu ya kwanza ya somo la pili la moduli ya Wajibu wa Raia. Tukutane katika sehemu inayofuata.

## Aina Mbalimbali za Ajali

Ndugu mwanafunzi, karibu sana katika sehemu hii ya pili katika somo la pili.

Kwanza, rejea orodha ya matukio ya huduma ya kwanza uliyoyaelezea katika sehemu ya kwanza ya somo hili, pamoja na picha namba 4 na 5. Ni wazi kwamba zipo aina mbalimbali za ajali. Baadhi yake zinaweza kuwa zifuatavyo:

- majeraha madogomadogo ya kuungua na moto, maji, mafuta na kadhalika;
- majeraha makubwa yatokanayo na kuungua na kemikali;
- Majeraha madogomadogo ya kukatwa na vitu vyenye makali;
- kuumwa na nyoka;
- kuumwa na wadudu;
- kukosa hewa;
- kutoka damu puani;
- michubuko;
- kuvunjika mfupa au mifupa;
- kuzama kwenye maji; na
- kuanguka kutoka juu kama vile juu ya mti, paa; ukuta n.k

Tafadhali ongeza aina nyingine zaidi, ambazo hazikutajwa.

Ndugu mwanafunzi, hapa umefika mwisho wa sehemu ya pili ya somo la pili la moduli ya Wajibu wa Raia. Jitayarishe kuanza sehemu inayofuata.

## Hatua za Huduma ya Kwanza

Ndugu mwanafunzi, karibu sana katika sehemu hii ya tatu katika somo la pili la Moduli ya Wajibu wa Raia'. Tafadhali fanya yafuatayo:

Tembelea hospitali au kituo cha afya kilichopo karibu na eneo lako ili uweze kupata maelekezo ya hatua zipi za kuchukua kwa kila aina ya ajali iliyoorodheshwa katika sehemu ya pili ya somo la pili.

Yaweke maelezo yako katika mpangilio ufuatao na kuyaweka katika mkoba wa kazi (rejea mfano uliotolewa):

Hatua za kuchukua kwa kila aina ya ajali

| Namba | Aina ya ajali | Hatua ya kuchulua |
|---|---|---|
| 1. | Majeraha madogomadogo ya kuungua na moto, maji, mafuta na kadharika | Weka jeraha mara moja (haraka) katika maji masafi ya baridi kwa muda upatao dakika kumi. |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| 11. | | |
| 12. | | |
| 13. | | |
| 14. | | |
| 15. | | |

Jambo la kuzingatia, ni kumpeleka mwathirika/mgonjwa hospitalini au kituo cha afya haraka iwezehanavyo, hasa, pale athari inapokuwa kubwa. Wakati wote wa huduma ya kwanza na safari ya kumpeleka hospitalini, mgonjwa atiwe moyo na matumaini ya kupona.

Maelezo ya hatua za kuchukua kwa kila aina ya ajali, yatakuwa yamekufikisha mwisho wa sehemu ya tatu katika somo la pili la Moduli ya Wajibu wa Raia. Sasa uko tayari kuanza sehemu ya nne ya somo la pili.

## Vifaa vya Huduma ya Kwanza

Ndugu mwanafunzi, karibu sasa katika sehemu hii ya nne katika somo la pili la Moduli ya Wajibu wa Raia.

Kwa kurejea jedwali lako la taarifa ya hatua za kuchukua wakati ajali inapotokea (sehemu ya tatu ya somo), orodhesha vifaa muhimu vinavyohitajika katika huduma ya kwanza kwa kila aina ya ajali. Andika orodha hiyo kwa kutumia jedwali. (Angalia mifano ifuatayo).

Vifaa muhimu vinavyohitajika katika huduma ya kwanza kwa kila aina ya ajali

| Na. | Aina ya ajali | Vifaa muhimu vinavyohitajika |
|---|---|---|
| 1. | Majeraha madogo madogo ya kuungua na moto, maji, mafuta na kadharika | Maji baridi |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | Kuumwa na nyoka | Wembe/kisu kikali, kamba |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| 11. | | |
| 12. | | |
| 13. | | |
| 14. | | |
| 15. | | |

Ndugu mwanafunzi, jedwali lako la vifaa muhimu vinavyohitajika katika huduma ya kwanza kwa kila aina ya ajali, litakuwa limekufikisha mwisho wa sehemu ya nne katika somo la pili la

Moduli ya Wajibu wa Raia. Sasa jiweke tayari kuanza sehemu ya tano ya somo la pili.

## Jinsi ya Kutumia Vifaa vya Huduma ya Kwanza

Tafadhali, rejea orodha ya vifaa muhimu vinavyohitajika katika huduma ya kwanza kwa kila aina ya ajali.

Ili kurahisisha utoaji huduma ya kwanza kwa wakati mwafaka, ni wazi kwamba baadhi ya vifaa hivyo ni vema vikahifadhiwa sehemu moja maalumu. Kwa ajili hiyo, huwa kuna kifaa kijulikanacho kama 'Kisanduku cha Huduma ya Kwanza'. Mara nyingi, kifaa hiki hupatikana katika shule zenye uongozi makini; mabasi yanayojali abiria wake; vituo vya afya; na majumbani ambako kuna wanafamilia wanaoelewa umuhimu wake.

Kwa kawaida, kisanduku hiki kinatengenezwa kwa mbao. Vifaa vinavyowekwa humo ni kama vifuatavyo:

- Mkasi
- Aina mbalimbali za bendeji
- Pamba
- Nyembe mpya
- Glovu
- Gundi ya karatasi
- Mafuta ya vaselini
- Dawa za kupaka kwenye vidonda
- Sabuni ya kunawa mikono
- Dawa ya kusafishia vidonda
- Vidonge vya kupunguza maumivu, kama vile Panado na Parasetamo
- Spiriti
- Madini joto (ayodini)
- Maji safi ya kunywa (mfano ya chupa, ambayo yatafaa zaidi kusafishia majeraha pia)

Baada ya kuona orodha ya vifaa ndani ya kisanduku cha huduma ya kwanza:

1. Vifaa hivyo vinaweza kuhifadhiwa katika chombo gani kingine, tofauti na kisanduku cha mbao? Chagua vifaa vinavyoweza kufaa kati ya vilivyotajwa ndani ya kisanduku kifuatacho.



**Kabati la vyombo**



Ndoo ya plastiki



Kabati la nguo



Sanduku la nguo

2. Tahadhari gani zitakupasa kuchukua utakapokuwa

3. umeanzisha kisanduku chako cha familia au kijiji? Jadili na wanafunzi wenzako walio karibu nawe au marafiki na jamaa. Pia waulize wataalam wa afya katika eneo unaloishi.

4. Kufuatana na hali ya mahali unapoishi, anzisha kisanduku cha huduma ya kwanza kwa kuwasiliana na afisa afya aliye karibu nawe, na uanze kulitumia.




Jinsi ya kuufunga mguu uliovunjika



Mtu aliyevunjika mkono



Mtu aliyevunjika uti wa mgongo



**Mtu aliyezama majini na kunywa maji mengi**

Ndugu mwanafunzi, tafadhali sasa fanya yafuatayo:

---

Anzisha kisanduku cha huduma ya kwanza kisha kitumie ndani ya familia yako na jamii inayokuzunguka.

---

Baada ya kuanzia kisanduku cha huduma ya kwanza umekamilisha somo hili la kutoa huduma ya kwanza pale ajali inapotokea. Umahiri wa kutoa huduma ya kwanza utaendelea kuimarika kadri unavyotoa huduma hiyo.

## Tafakuri

Katika somo zima umejifunza mambo gani? Katika somo hili Kipengele kipi kimekuwa kivutio zaidi kwako na kwa nini? Wapi umekutana na ugumu wa kujifunza ndani ya somo hili? Ni hatua gani umechukua au utachukua ili kuweza kupata ufumbuzi wa tatizo au matatizo yako?

# Zoezi

Ndugu mwanafunzi, bila shaka sasa unaweza kujipima kama matokeo ya mafunzo yaliyokusudiwa yameweza kufikiwa kufuatana na mwongozo ufuatao:

Ninaweza:

1. kuwaeleza watu wengine dhana ya huduma ya kwanza kwa usahihi. Kwa kifupi, huduma hii ni......................................
   ..........................................................................;

2. kuainisha aina mbali mbali za ajali. Kwa mfano: ....................
   ..........................................................................
   ..........................................................................; na

3. kuanzisha kisanduku cha huduma ya kwanza na kutoa huduma ndani ya familia yangu na jamii inayonizunguka. Kwa mfano nitatumia kisanduku cha .......na kuweka ndani yake:
   - ........................... kwa ajili ya ..................................
   - ........................... kwa ajili ya ..................................
   - ........................... kwa ajili ya ..................................
   - ........................... kwa ajili ya ..................................

# Somo la Tatu

## Kufafanua Madhara ya Dawa za Kulevya na Namna ya Kuepukana Nazo

### Utangulizi

Ndugu mwanafunzi, karibu sana katika somo la tatu la Moduli ya Elimu ya Uraia. Bila shaka, umewahi kusikia mara nyingi redioni, magazetini na katika luninga habari za watu waliokamatwa na vyombo vya dola kwa tuhuma za, aidha, kusafirisha dawa za kulevya; kulima mazao yaliyo katika kundi la dawa za kulevya, kwa mfano bangi, au kuyatumia.

Hii ina maana tatizo la utumiaji wa dawa za kulevya nchini mwetu Tanzania ni kubwa. Licha ya kuwa utumiaji wa dawa hizi ni kosa la jinai, madhara yake kwa mtumiaji na ustawi wa jamii nzima ni makubwa pia. Hivyo, kila raia mwema ana wajibu wa kupiga vita matumizi ya dawa za kulevya. Ili kufanikisha vita hii, watu wanahitaji kuwa na umahiri katika kuubainisha utumiaji wa dawa hizo; madhara yake; na namna ya kuepukana nazo. Somo hili linalenga kukupatia umahiri huo.


## Matokeo ya Kujifunza

Ndugu mwanafunzi, baada ya kumaliza kujifunza somo hili, unakusudiwa uwe umepata umahiri katika maeneo yafuatayo:

- kubainisha dhana ya dawa za kulevya;
- kueleza madhara ya dawa za kulevya kwa mtumiaji na jamii kwa ujumla; na
- kubainisha njia za kuepuka utumiaji wa dawa za kulevya.

## Dhana ya Dawa za Kulevya

Ndugu mwanafunzi, kulingana na habari ulizokwisha kuzisikia kuhusiana na dawa za kulevya, unadhani dawa hizi ni zipi na zinatumikaje? Jadili swali hili na marafiki, ndugu au jamaa na majibu yake uyaweke katika mkoba wako wa kazi. Baada ya hapo, jaribu, pia, kuujaza utando wa buibui ufuatao juu ya dhana ya dawa za kulevya. Mifano imetolewa. Unaweza kuongeza zaidi.




Nina hakika kwa kukamilisha utando huu wa buibui, utakuwa umeweza kujenga umahiri wa kueleza dhana ya madawa ya kulevya.

## Madhara ya Dawa za Kulevya

Ndugu mwanafunzi, katika sehemu ya kwanza ya somo umepata dhana ya dawa za kulevya na baadhi ya aina zake, hasa zile zinazotumiwa zaidi kinyume cha sheria kwa madhumini ya mtu kujilewesha, au kupumbaza akili yake. Yafuatayo ni baadhi ya madhara yanayoweza kutokana na utumiaji wa dawa za kulevvya:

- kuvurugika au kuchangayikiwa;
- mtumiaji kuwa mwizi au jambazi;

- ugomvi na/au mauaji kutokea;
- maendeleo ya masomo hushuka;
- kukosa hamu ya kula na kukonda/kudhoofu;
- kama mtumiaji ni dereva anaweza kusababisha ajali nyingi barabarani;
- kupata UKIMWI;
- kutofanya kazi;
- kutumia vibaya rasilimali; na
- kupoteza muda bila kufanya shughuli za maendeleo.

---

Kati ya madhara haya ni madhara gani yanaathiri jamii inayomzunguka mtumiaji? Kwa namna gani?

---

Ndugu mwanafunzi, baada ya kuona mifano hii ya madhara ya dawa za kulevya sasa:

- fanya uchunguzi katika eneo unaloishi uone ni kwa kiasi gani tatizo la dawa za kulevya lipo. Onyesha pia sababu zake na hatua zinazochukuliwa kupuguza tatizo hilo;
- chunguza majina ya dawa hizo yanayotumika mtaani; na namna yanavyosambazwa/uzwa; na
- jadili na wanamafunzo wenzako au marafiki na jamaa juu ya hatua mnazoweza kuchukua kusaidia kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya katika jamii yenu na nchi kwa ujumla.

Ndugu mwanafunzi, baada ya kufanya kazi hii, utakuwa umemaliza sehemu ya pili ya somo la pili la Moduli ya Wajibu wa Raia. Tukutane katika sehemu inayofuata.

## Kubainisha Njia za Kuepuka Utumiaji wa Dawa za Kulevya

Ndugu mwanafunzi, karibu tena katika sehemu hii ya tatu na ya mwisho katika somo la tatu la moduli ya 'Wajibu wa Raia'.

Baada ya kuona madhara ya dawa za kulevya, hebu sasa tuone njia zilizokwisha fanyiwa utafiti na kugundulika zinafaa katika kuepusha vijana kushiriki utumiaji wa dawa za kulevya, njia hizo ni pamoja na:

1. kuwa na elimu ya kutosha juu ya dawa za kulevya na athari zake;

2. kuepuka kukaa bila shughuli;

3. kuepuka makundi mabaya yanayoweza kumshawishi mtu, hasa kijana, kujihusisha na dawa za kulevya; na

4. kushiriki katika vilabu vya vijana vinavyojihusisha na uzalishaji mali pamoja na kutoa elimu ya stadi za maisha.

Jadili na wanamafunzo wanzako walio karibu nawe au marafiki na jamaa juu ya njia hizi muone ni kwa kiasi gani zinafaa katika sehemu mnayoishi. Njia zipi nyingine zinaweza kutumika?

Ndugu mwanafunzi, utakuwa umekamilisha sehemu hii ya mwisho katika somo la tatu la Madhara ya Dawa za Kulevya, na namna ya kuepukana nazo. Fanya majadiliano na kuandika ripoti fupi. Vilevle, umefika tamati ya Moduli ya Pili ya Wajibu wa Raia.

## Tafakuri

Kwa tafakari ya somo zima, jibu maswali yafuatayo:

1. Je, ni mambo gani umejifunza katika somo zima?
2. Ni kipengele kipi katika somo hili kimekuwa kivutio zaidi kwako na kwa nini?
3. Je ni wapi umekutana na ugumu wa kujifunza ndani ya somo hili? Ni hatua gani umechukua au utachukua ili kuweza kupata ufumbuzi wa tatizo au matatizo yako?

## Zoezi

Ndugu mwanafunzi, bila shaka sasa unaweza kujipima kama matokeo ya mafunzo yaliyokusudiwa yameweza kufikiwa kufuatana na mwongozo ufuatao:

Ninaweza:

1. kuwaeleza watu wengine dhana ya dawa za kulevya kwa usahihi.

   Kwa kifupi, huduma hii ni.........................................

   ..........................................................................

2. Kueleza madhara ya dawa za kulevya kwa mtumiaji na jamii kwa ujumla

   Kwa mfano: ........................................................

   ..........................................................................

   ..........................................................................

3. Kubanisha njia za kuepuka utumiaji wa dawa za kulevya na kuzitumia:

   Kwanza:..............................................................

   Pili: ..................................................................

   Tatu: ..................... ..........................................

# Somo la Nne

## Kubainisha Misingi ya Utawala Bora na Maadili

### Utangulizi

Ndugu mwanafunzi, karibu sana katika somo la nne la Moduli ya Wajibu wa Uraia. Utawala bora unaambatana na uongozi bora, ambao ni moja ya mambo muhimu yanayohitajika ili nchi yoyote ile duniani iendelee. Mambo mengine ni watu, ardhi na siasa safi, kama ambavyo Mwalimu J. K. Nyerere, Baba wa Taifa letu la Tanzania, alivyokuwa akisisitiza

Katika nchi yetu, utawala upo, na unaanzia ngazi ya nyumba au kaya moja, yaani familia, na kuendelea ngazi ya nyumba kumi, mtaa au kijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa hadi taifa. Kwa vile kila Mtanzania mwenye akili timamu ana fursa sawa ya kuwa kiongozi/mtawala katika ngazi zote tulizoziona, ina maana kila mmoja hana budi kuwa na umahiri wa kutosha katika eneo hilo. Somo hili linalenga kuwezesha upatikanaji wa umahiri huo.

## Matokeo ya kujifunza

Ndugu mwanafunzi, baada ya kumaliza kujifunza somo hili, unakusudiwa uwe umepata umahiri katika maeneo yafuatayo:

- kueleza dhana ya utawala bora;
- kubanisha misingi ya utawala bora;
- kueleza dhana ya maadili ya uongozi;
- kuainisha misingi ya maadili ya uongozi bora; na
- kutathmini hali ya utawala bora na maadili ya uongozi katika jamii.

*Kueleza Dhana ya Utawala Bora*

Ndugu mwanafunzi, karibu katika sehemu hii ya kwanza katika somo la nne la Moduli ya Wajibu wa Raia.

Ukiondoa mkuu wa nchi wa wakati uliopo, kila mtu yupo chini ya utawala na uongozi fulani, yaani ngazi zote zilizotajwa katika utangulizi wa somo. Hata mtoto mdogo naye huwa yupo chini ya utawala na uongozi wa baba na mama au mzazi mmojawapo peke yake, pia ndugu zake wakubwa kwa wakati fulani. Vijana nao huanza kwa kuwaongoza wadogo zao, wenzao madarasani, katika vilabu vya michezo mbalimbali, n.k. Hivyo, ni wazi kuwa kila mtu anao uzoefu wa kutawaliwa na kuongozwa au kutawala na kuongoza.

Kwa kutumia uzoefu wako wa utawala na uongozi utawala bora kwako ni utawala wa namna gani?

Jadili swali hili na marafiki, ndugu au jamaa na majibu yake uyaweke katika mkoba wa kazi.

Labda jibu lako halitakuwa mbali na hili:

Utawala bora ni pale viongozi wanapotimiza wajibu na majukumu kwa kuzingatia nakuheshimu haki za binadamu.


Ndugu mwanafunzi, hapa umefikia mwisho wa sehemu hii ya kwanza katika somo la nne la moduli ya Wajibu wa Raia. Jitayarishe kuingia katika sehemu inayofuatia.

## Kubanisha Misingi ya Utawala Bora

Ndugu mwanafunzi, Tafadhali rejea dhana ya utawala bora. Mara nyingi, mahali palipo na utawala bora ipo misingi inayoongoza utawala wa namna hiyo, na inafuatwa kwa vitendo.

Jadili usemi huu na marafiki, ndugu au jamaa na matokea yake uyaweke katika mkoba wa kazi.

Kwa kutumia uzoefu wako, hasa ule wa kutawaliwa, jaza utando wa buibui ufuatao juu ya misingi ya utawala bora. Mifano imetolewa. Unaweza kuongeza vyumba zaidi.




Bila shaka, kwa kukamilisha utando wa buibui, utakuwa umeweza kujenga umahiri wa kubainisha misingi ya utawala bora.

Je, utautumiaje katika maisha yako?

Ndugu mwanafunzi, baada ya kuwa umejaza utando wa buibui na kujibu swali ulilooulizwa, utakuwa umekamilisha sehemu hii ya pili katika somo la nne la moduli ya Wajibu wa Raia. Karibu katika sehemu inayofuata.

## Kueleza Dhana ya Maadili ya Uongozi

Ndugu mwanafunzi, karibu katika sehemu ya tatu katika somo la nne la Moduli ya Wajibu wa Raia.

Neno maadili lina maana ya mambo yanayoongoza au kutawala mwenendo na tabia ya mtu katika kufanya kazi fulani na/au kuishi katika jamii fulani.

Hebu eleza tofauti ya mwenendo wako ukiwa sehemu ya:

- ibada;
- michezoni na wenzako;
- ukiwa na wazazi wako; na
- ukiwa na walimu wako.

Kwa nini unaenenda tofauti tofauti katika sehemu zote hizo? Jadili.

Baada ya kujadili, weka maelezo yako katika mkoba wa kazi.

Ndugu mwanafunzi, baada ya kufanya kazi hii, utakuwa umemaliza sehemu ya tatu katika somo la nne la Moduli ya Wajibu wa Raia.


## Kuanisha Misingi ya Maadili ya Uongozi Bora

Ndugu mwanafunzi, karibu katika sehemu hii ya nne katika somo la nne la moduli ya 'Wajibu wa Raia'.

Tafadhali rejea dhana ya maadili ya uongozi. Kama ilivyo kwa utawala bora, mahali palipo na uongozi bora, vile vile, ipo misingi inayoongoza uongozi wa namna hiyo.

Jadili usemi huu na marafiki, ndugu au jamaa na matokeo yake uyaweke katika mkoba wa kazi.

Baada ya hapo, na kwa kutumia uzoefu wako, hasa ule wa kuongozwa, jaza utando wa buibui ufuatao juu ya misingi ya uongozi bora. Mifano imetolewa. Unaweza kuongeza vyumba zaidi.




Nina hakika kwa kukamilisha utando huu wa buibui, utakuwa umeweza kujenga umahiri wa kuainisha misingi ya utawala bora.

- Toa maoni yako juu ya viongozi wa umma katika jamii kuhusiana na misingi ya uongozi bora.
- Je, umahiri ulioupata utakusaidiaje katika maisha yako?

Ndugu mwanafunzi, baada ya kuwa umejaza utando wa buibui na kujibu maswali uliyoulizwa, utakuwa umekamilisha sehemu hii ya tatu katika somo la nne la moduli ya Wajibu wa Raia.

## Kutathmini Hali ya Utawala Bora na Maadili ya Uongozi katika Jamii

Ndugu mwanafunzi, sehemu hii itakuhusisha zaidi na kazi ya utafiti mdogo unaolenga kukuwezesha kupima ni kiasi gani misingi ya utawala bora na maadili ya uongozi inafuatwa kwa vitendo katika jamii unamoishi.

Hebu fikiria na upange njia za kufuata, na vifaa vya kutumia.

Ili kuweza kufikia uamuzi ni vema ukaanza na aina ya taarifa unazohitaji kuzipata toka katika jamii. Ni wazi utahitaji kupata habari kuhusiana na kila kipengele cha misingi ya utawala na uongozi bora. Habari hizo unaweza kuzipata kwa njia zifuatazo:

1. Dodoso: maswali yenye chenye vipengele vya kujaza taarifa zilizowekewa nafasi wazi kwa ajili ya mlengwa kujaza taarifa anayoelekezwa. Linakuwa na sehemu kuu mbili: **i.** Taarifa binafsi; na **ii.** Taarifa za masuala

Mfano:

**Dodoso la Raia wa Kawaida**

**Hali ya Utawala Bora na Maadili ya Viongozi Katika Kata ya Songambele**

i. **Taarifa binafsi**

Mtaa wa: .....................................

Kata ya: ........................................

Wilaya ya: .........................................

Tarehe: ..................................................

Jina .........................................(Ukipenda)

Jinsi: Me: ................. Ke: ......................

Umri: .......................

Kiwango cha elimu

Hebu taja

ii. **Taarifa za masuala**

1. Unaelewa nini kuhusu misingi ya utawala bora na maadili ya viongozi?

   ......................................................................

   ......................................................................

2. Ni misingi ipi ya utawala bora na maadili ya viongozi inatekelezwa vema katika ngazi tofauti za uongozi katika kata yako?

   ......................................................................

   ......................................................................

3. Ni matukio yapi katika kata hii yanaweza kujitokeza kwa sababu ya kukiukwa kwa misingi ya utawala bora na maadili ya viongozi? Tafadhli yataje na kuyaeleza kwa kifupi.

Ndugu mwanafunzi, zaidi ya dodoso, unaweza kutumia orodha ya maswali ya siri, ambayo utakuwa ukiyafuata katika kuuliza, maswali anajibu wewe unaandika anachojibu. Kingine ni orodha ya mambo ya kuchuguza kwa kuangalia kwa macho.

Kwa mfano:

1. Viongozi wanatumia magari ya ofisi kupeleka wake au waume zao saluni na madukani?
2. Baadhi ya viongozi wanadai rushwa ili kumpatia mtu huduma?
3. Wananchi wanatambua matukio ambapo maadili yanakuwa yamekiukwa?
4. Wananchi wanafanya nini mahali ambapo maadili yamekiukwa?

Kwa kutumia mifano hii, tayarisha vifaa hivyo na kuvitumia kukusanya habari katika kata unayoishi juu ya aidha hali ya utawala bora au maadili ya viongozi. Hiyo taarifa itumie kuandika ripoti fupi ya matokeo na iwe na mapendekezo ya kuboresha hali hiyo. Si lazima uwaulize watu wote, ila chukua asilimia isiyopungua thelathini (30%).

Ripoti yako ndiyo itakuwa imekufikisha tamati ya sehemu ya nne na ya mwisho katika somo la pili la Moduli ya Wajibu wa Raia.

## Tafakuri

Tafadhali tafakari kwa makini somo zima kwa kutumia maswali yafuatayo:

a) Je, umejifunza mambo gani katika somo zima?

b) Kipengele kipi katika somo hili kimekuwa kivutio zaidi kwako? Unadhani ni kwa nini?

c) Je ni wapi umekutana na ugumu wa kujifunza somo hili? Umechukua au utachukua hatua gani kupata ufumbuzi wa tatizo au matatizo yako?

## Zoezi

Ndugu mwanafunzi, bila shaka sasa unaweza kujipima kama matokeo ya mafunzo yaliyokusudiwa yameweza kufikiwa kufuatana na mwongozo wa maswali yafuatayo:

1. Ninaweza kuelezea dhana ya 'utawala bora' na 'maadili ya uongozi' bila msaada.

   ....................................................................

   ....................................................................

   ....................................................................

   ....................................................................

2. Ninaweza kubainisha utawala na uongozi unaofuata misingi ya utawala bora na maadili ya uongozi katika jamii

   Kati yake ni:

   i. ....................................................................

   ii. ....................................................................

   iii. ....................................................................

   iv. ....................................................................

3. Ninaweza kutathmini hali ya utawala bora na maadili ya uongozi katika jamii ninamoishi.

   Mfano nimegundua kuwa matukio: (asilimia)..... ................

   i. ...........................................................;

   ii. .......................................................; na.

   iii. ............................................................... yalitokana na kukiukwa kwa misingi ya utawala bora na maadili ya uongozi.

# Somo la Tano

## Kubainisha Misingi ya Utandawazi na Namna ya Kukabiliana na Changamoto Zake

### Utangulizi

Ndugu mwanafunzi, karibu sana katika somo la tano la moduli ya Wajibu wa Raia. Utandawazi ni jambo ambalo limekuja na maendeleo ya dunia na haliepukiki na nchi yoyote ile hata kama haiutaki. Kwa vile utandawazi huu una changamoto nyingi kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, ni vema kila raia aielewe misingi yake, awe na umahiri wa kuchanganua chagamoto zake na jinsi ya kukabiliana nazo ili taifa letu lisipoteze mwelekeo. Ni kutokana na sababu hizi, somo hili linalenga kuwezesha upatikanaji wa umahiri huo.

## Matokeo ya kujifunza

Ndugu mwanafunzi, baada ya kumaliza kujifunza somo hili, unakusudiwa uwe umepata umahiri katika maeneo yafuatayo:

- kueleza dhana ya utandawazi;
- kueleza chimbuko la utandawazi;
- kuchambua misingi ya utandawazi; na
- kuchanganua manufaa na changamoto za utandawazi njia za kukabiliana nazo.

#### Dhana ya Utandawazi

Ndugu mwanafunzi, dhana ya utandawazi inaweza kuelezewa kwa namna nyingi. Maelezo yanayotumika zaidi ni pamoja na haya:

1. hali ya kuongezeka kwa kutegemeana na kuingiliana kwa mataifa duniani kote katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi;

2. pale ulimwengu unapoonekana kuwa kama kijiji kimoja;

3. suala la mfumo ambapo watu wanafanya kazi pamoja kuendeleza/kupanua mitaji, bidhaa na taarifa bila kufungwa, au, kuzuiwa na mipaka ya mataifa yao.

   - ni mambo yapi yanarahisisha mwingiliano huo?
   - maneno kuonekana kama 'kijiji kimoja' yana maana gani?

Jadili maswali haya na marafiki, ndugu au jamaa na majibu yake uyaweke katika mkoba wa kazi.

Ndugu mwanafunzi, kwa kupata majibu ya maswali hayo mawili utakuwa umekamilisha sehemu hii ya kwanza katika somo la tano la Moduli ya Wajibu wa Raia. Bila shaka, itakusaidia katika kujifunza sehemu inayofuatia.

**_Chimbuko_ la Utandawazi**

Mpendwa mwanafunzi, karibu katika sehemu hii ya pili katika somo la tano la Moduli ya Wajibu wa Raia.

Tafadhali rejea dhana ya utandawazi. Utandawazi umejengeka kuanzia karne ya 15 ambayo ilisababishwa na kukua kwa biashara ya uchuuzi huko Ulaya, ambako wafanyabiashara walihitaji kupanua masoko na mitaji ila mipaka ya mataifa ilikuwa ni kikwazo kwa upanuzi huo. Hali hii unaweza kuiona katika ngazi yoyote ya jamii; kwa mfano, kata, wilaya au mkoa.

Katika sehemu unayoishi, au jirani yake, mtafute mtu aliye na biashara ya duka, nishati ya mafuta, huduma ya shule, hospitali na kadhalika ambaye amefungua tawi au matawi ya biashara/huduma ya aina hiyohiyo katika sehemu nyingine za mji, wilaya, mkoa au vyote vitatu.

- Ni sababu zipi zilimfanya afungue tawi/matawi hayo mahali pengine?
- Wafanyakazi katika matawi hayo wanaishi wapi na aliwapataje?
- Mapato yapatikanayo katika matawi hayo yanakwenda/yanapelekwa wapi?

Jadili na wahusika kisha majibu uyaweke katika mkoba wa kazi.

Mazingira yafuatayo ni kati ya yale yaliyosababisha biashara Ulaya kukua hadi kufikia hali ya kuhitajika upanuzi wa mitaji nje ya mipaka na watu kufanya kazi pamoja, kila mmoja akiwa nchini kwake:

1. biashara ya watumwa kati ya Afrika, Marekani na Ulaya, ambapo watu wa pande zote tatu waliunganishwa;
2. vita kuu ya dunia, ambayo iliunganisha mabara mengi zaidi;
3. maendeleo katika elimu, ambayo yamekuza sayansi na teknolojia na hali ya wasomi kusafiri na hivyo kukutana, na
4. kupanuka kwa demokrasia ambapo watu wameendelea kuwa huru zaidi kusafiri popote na kufanya mawasiliano

Ndugu mwanafunzi, kama utandawazi ni pamoja na mwingiliano wa watu katika nyanja za biashara na taarifa hebu chunguza yafuatayo:

- Chunguza mitandao ya aina hii iliyopo katika eneo unaliishi pia.
- Wewe na vijana wenzako au ndugu na jamaa mnawezaje kuwa sehemu yake?
- Jadili na marafiki, ndugu au jamaa na matokea yake uyaweke katika mkoba wa kazi.

Ndugu mwanafunzi, baada ya kuwa umekamilisha kazi hii utakuwa umemaliza sehemu hii ya pili katika somo la tano la Moduli ya Wajibu wa Raia.

## Misingi ya Utandawazi

Ndugu mwanafunzi, karibu katika sehemu hii ya tatu katika somo la tano la Moduli ya Wajibu wa Raia.

Kwanza, angalia hali halisi ilivyo nchini mwetu sasa hivi: inachukua muda kiasi gani kwa habari kuenea toka sehemu moja ya nchi, hata kama ni kjijini, na kuenea pote? Siku hizi unaweza kumsikia kiongozi wa nchi yupo hapa asubuhi, jioni yuko mji mwingine, kesho yupo ya nje ya nchi, na kesho kutwa yuko nchi nyingine na kurudi hapa nchini tena jioni.

Hebu eleza ni nini kilichowezesha hali hii?

Jadili swali hili na marafiki, ndugu au jamaa na matokea yake uyaweke katika mkoba wa kazi.

Baadhi ya majibu yako yanaweza kufanana na haya:

- kukua kwa sayansi ya usafiri;
- mapinduzi katika teknolojia ya habari na mawasiliano; na
- kukua na kuimarika kwa miundombinu ya usafiri wa anga na barabara.

Toa maelezo mafupi kufafanua kila moja ya majibu hayo matatu.

Ndugu mwanafunzi, baada ya kufanya kazi hii, utakuwa umemaliza sehemu ya tatu katika somo la nne la Moduli ya Wajibu wa Raia.

## Manufaa na Changamoto za Utandawazi

Ndugu mwanafunzi, sehemu hii itakuhusisha zaidi na kazi ya utafiti mdogo unaolenga kukuwezesha kukusanya maoni ya watu mbali mbali kuhusu manufaa na changamoto za utandawazi, njia za kukabiliana nazo, ngazi ya mtaa, kata unamoishi hadi taifa zima.

Kwanza fikiria na upange njia za kufuata, na vifaa vya kutumia. Ili uweze kufikia uamuzi juu ya haya, chagua aina ya taarifa unazohitaji kuzipata toka katika jamii. Kwa mfano:

1. habari kuhusiana na manufaa ya utandawazi;
2. habari kuhusiana na changamoto za utandawazi;
3. habari kuhusiana na maoni ya jinsi ya kukabiliana na utandawazi.

Habari hizo unaweza kuzipata kwa kutumia:

1. Dodoso;
2. Orodha ya maswali ya usiri; na
3. Orodha ya mambo ya kuchuguza kwa kuangalia kwa macho.

Mfano: Tumia mifano iliyopo katika somo la pili la moduli ya kwanza ('Haki za Binadamu'), sehemu ya tatu; na somo la nne la moduli ya pili ('Wajibu wa Raia'), sehemu ya nne.

Kwa kutumia mifano uliyoelekezwa, tayarisha vifaa hivyo na kuvitumia kukusanya habari katika mtaa, kata na/au wilaya unamoishi juu ya manufaa na changamoto za utandawazi na njia za kukabiliana nazo. Taarifa hiyo itumie kuandikia ripoti fupi ya matokeo yenye mapendekezo ya kuboresha. Si lazima uwaulize watu wote, ila chukua asilimia isiyopungua thelathini (30%).

Ripoti yako ndio itakayokufikisha kwenye tamati ya sehemu ya nne na ya mwisho katika somo la tano la Moduli ya Wajibu wa Raia ambalo ni somo la mwisho pia.

## Tafakuri

Tafadhali tafakari kwa makini somo zima kwa kutumia maswali yafuatayo:

1. Je, ni mambo gani umejifunza katika somo zima?
2. Ni kipengele kipi katika somo hili kimekuwa kivutio zaidi kwako? Unadhani ni kwa nini?
3. Je, ni wapi umekutana na ugumu wa kujifunza somo hili? Ni hatua gani umechukua au utachukua ili kuweza kupata ufumbuzi wa tatizo au matatizo yako?

## Zoezi

Ndugu mwanafunzi, bila shaka sasa unaweza kujipima kama matokeo ya mafunzo yaliyokusudiwa yameweza kufikiwa kufuatana na mwongozo wa maswali yafuatayo:

1. Ninaweza kuelezea dhana 'utandawazi' bila msaada.

   Kwa kifupi utandawazi ni: ……….........................................

   ……………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………

2. Ninaweza kueleza chimbuko la utandawazi

   Kati yake ni:

   i. ……………………………………………………………………

   ii. ……………………………………………………………………

   iii. ……………………………………………………………………

3. Ninaweza kuchambua misingi ya utandawazi.

   Mfano: ………………..……………………..…………………..…

   i. ……………………………………………………………………;


   ii. ……………………………………………………………………;

   iii. ……………………………………………………………………

## Marejeo

Manzi, Z. M. (2007). **Civics for Secondary Schools, Book Four** Dar es Salaam: PBL Publishers.

# INTEGRATED POST PRIMARY EDUCATION PROGRAMME



unicef
unite for children

**Elimu Changamani baada ya Elimu ya Msingi**

INSTITUTE OF ADULT EDUCATION
EDUCATION HAS NO END